

Kifua kikuu

Taarifa kwa wagonjwa kutoka kwa daktari wa magonjwa ya kuambukiza nchini Uswidi.

Kwa nini nimepokea taarifa hii?

Una ugonjwa wa kifua kikuu au unashukiwa kuwa nao, na unahitaji matibabu. Karatasi hii inatoa taarifa kuhusu kifua kikuu, jinsi ugonjwa unavyotibiwa na unachohitaji kufanya.

Kifua kikuu ni nini?

Kifua kikuu (pia huitwa TBC au TB) ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na bakteria, *Mycobacterium tuberculosis*. Dalili za ugonjwa mara nyingi huonekana muda mrefu (miezi au miaka) baada ya kuambukizwa. Mara nyingi mtu hupata nimonia, lakini sehemu zingine za mwili pia zinaweza kuathiriwa, kama vile tezi za limfu, utando wa mapafu, mfumo wa mifupa, ubongo au figo.

Kifua kikuu huambukizwaje?

Ugonjwa huu huenezwa na watu wenye kifua kikuu kwenye mapafu yao. Bakteria zinasambaa kupitia hewa ndani ya nyumba mtu anapokohoa na mtu mwingine anavuta matone madogo yenye bakteria. Kifua kikuu huambukizwa hasa ukiwa karibu na mtu mgonjwa kwa muda mrefu. Ni nadra kwa mtu kuambukizwa kupitia kuonana na mgonjwa kwa muda mfupi au mara moja moja.

Unajuaje kama una kifua kikuu?

Dalili hutegemea mahali ambapo bakteria za kifua kikuu hupatikana mwilini. Dalili za kawaida ni kikohozi kinachodumu kwa zaidi ya wiki 3, kutoa jasho usiku, homa na kupungua uzito. Dalili zingine zinaweza kujumuisha uvimbe (kifua kikuu cha limfu) au maumivu (kifua kikuu cha mifupa au tumbo).

Kifua kikuu huambukiza kiasi gani?

Watu wenye kifua kikuu cha mapafu, ambapo bakteria zinapatikana kwenye makohozi, wanaweza kuambukiza sana kabla ya matibabu kuanza. Uwezo wa kuambukiza hupungua haraka katika wiki chache za kwanza za matibabu. Watu wenye kifua kikuu nje ya mapafu hawaambukizi. Watoto wadogo wenye kifua kikuu karibu hawaambukizi kamwe. Kifua kikuu hakienezwi kupitia nguo au vitu vingine. Ugonjwa huo huambukiza mara chache sana mkiwa nje.

Kifua kikuu ni hatari?

Kifua kikuu kisichotibiwa kinaweza kuleta madhara makubwa na wakati mwingine kinahatarisha maisha. Watoto wadogo na watu walio na kinga dhaifu ya mwili wako hatarini kuugua sana kutokana na kifua kikuu.

Kifua kikuu hutibiwaje?

Kifua kikuu hutibiwa kwa dawa zinazoua bakteria zinazosababisha ugonjwa huo. Matibabu yanaweza kudumu kwa miezi kadhaa. Ni muhimu sana ufuate matibabu ambayo daktari wako amekupatia.

Pia ni muhimu usikose vidonge vyovyote katika matibabu yako. Usipotumia dawa mara kwa mara, bakteria zinaweza kuwa sugu na ugonjwa utakuwa mgumu zaidi kutibu.

Unapata dawa na ziara za huduma ya afya bila malipo.

Ninapaswa kuzingatia nini ili kuepuka kuwaambukiza wengine?

Kifua kikuu ni ugonjwa unaochukuliwa kuwa hatari kwa umma kulingana na Sheria ya Kudhibiti Magonjwa Yanayoambukiza. Kwa hiyo, unatakiwa kufuata masharti fulani utakayopewa na daktari wako, yanayoitwa masharti ya kufuata. Mlezi wa mtoto ana jukumu la kuhakikisha kwamba mtoto anafuata masharti hayo.

Huenda ukahitaji kulazwa hospitalini kwa muda fulani ili kuepuka kuambukiza wengine.

Masharti ya kufuata

- Ikiwa una kifua kikuu kinachoambukiza, huruhusiwi kwenda kazini, shuleni au kwenye shughuli za burudani.
- Ni lazima uje kwa ziara za ufuatiliaji ikiwa daktari wako atakuambia uje.

Ninatakiwa kufuata masharti haya kwa muda gani?

Unapaswa kufuata masharti mpaka daktari wako atakaposema huambukizi tena.

Je, unafikiri masharti ya kufuata uliyopewa si sahihi?

Unaweza kudai kwamba uamuzi kuhusu masharti ya kufuata uchunguzwe tena na daktari wa kudhibiti magonjwa ya kuambukiza katika mkoa wako. Unafanya hivyo kwa kuwasiliana na daktari wa kudhibiti magonjwa ya kuambukiza katika mkoa wako.

[Taarifa ya mawasiliano kwa daktari wa magonjwa ya kuambukiza | Chama cha Madaktari wa Magonjwa ya Kuambukiza \(slf.se\)](#)

Unaweza pia kuwasiliana na daktari wa magonjwa ya kuambukiza kwa kupiga simu kwenye namba kuu ya huduma za afya katika mkoa wako.

Kabla ya uchunguzi huo kukamilika, unatakiwa kufuata masharti uliyopewa.

Ufuatiliaji wa maambukizi

Kulingana na Sheria ya Kudhibiti Magonjwa Yanayoambukiza, lazima ushiriki katika ufuatiliaji wa maambukizi. Hii ina maana kwamba lazima utoe taarifa kwa wataalamu wa afya ili waweze kujua ni lini, wapi na jinsi gani umeambukizwa na kama umewaambukiza wengine. Mambo unayosema ni ya siri (hayaruhusiwi kufichuliwa). Ni muhimu sana kupata watu wenye kifua kikuu ili wapatiwe matibabu. Mtu anaweza kuwa ameambukizwa lakini si lazima awe mgonjwa.

Taarifa zaidi

[Tuberkulos – tbc | 1177 \(1177.se\)](#)

